JUA

GAZETI LA MAENDELEO

Kiongozi: Mutiri-wa-Bashara - Mwaka wa 21 - Toleo la 445

Bukavu

Ni nani anayewasha moto kunako ISDR ?

Kiliweza kupita katika hali ya uwasiwasi na woga kufwatana na mzozo pia fujo kali iliyofanyika kati ya wanafunzi, walimu na kiongozi wa chuo, ndugu Lubilanji. Siku ile, mwalimu mkuu na kiongozi mkuu wa ISDR, ndugu Lubilanji katekwa nyara na wanafunzi wake, kapigwa makonde na pia katembezwa kama mwizi na mjambazi barabarani akitoa machozi na kuzomewa na wapitanjia wote. Askarijeshi wakisaidiwa na wanafunzi wa moyo mwema na wa huruma ndio wameweza kuepusha kifo, ndugu Lubilanji kwa kuwa shabaa ya wanafunzi hao ilikuwa ya kumtupa kiongozi wao katika maji ya ziwa Kivu kiisha kumfezehesha barabarani kote, wakipitia mitaani Ibanda, Bagira na Kadutu.

Kufwatana na maneno kakamilisha wanafunzi hao wakorofi, wasio na adabu ao huruma kwa wakubwa wao, mwalimu ama profesa Lubilanji ni mpokonyaji wa feza za ujenzi bora wa masomo yao. Ni ndipo wanafunzi kamustaki kiongozi huo kuwa ni yeye arudishae chuo chao nyuma kwa kuwa roho yake ni yakuchukia maendeleo na maisha ya kidemokrasia jimboni mwa Kivu ya Kusini na hasa shuleni ISDR/Bukavu. Akichukua usemi kunako mkutano uliyoongozwa na ndugu Modeste Musamba Kiyana Na-Bana, prezidenti wa kamati kuu iliyoundwa kwa kumalizisha fujo kunako chuo cha ISDR na ambae pia ni mnyampara mdogo wa mji wa Bukavu, mwanafunzi mmoja, ndugu Bashizi katoa mwangaza kamili kuhusu makosa waliyomshtaki kiongozi wao mkuu.

Makosa yale ni yafwatao. Kwanza: upokonyaji wa feza zilizotolewa na serkali kwa kuwalipa wanafunzi "bourses" yao ya majifunzo bora. Pili : kujiruhusu kutumikisha gari 2 ya ISDR, kama mali ya wazazi wake ingawa gari hizo chuo imezipewa na shirika la Unicef kwa kuwasaidia wanafunzi katika shuruli zao mbalimbali. Tatu : kuuza gari lingine "MAN" kwa watu kimagendo na kuficha pesa alizopewa kiisha mambo hayo kupitika. Inne : kukataa kuwaazibu wezi wawili waliyonaswa wakiisha kuuza chombo cha kuingiza moto wa stimu ingawa chombo chenyewa ilikua mali ya ISDR. Tano : kuwaandika hovyo hovyo wanafunzi akiombaomba rushwa na hata kuwageuza wabinti wamoja kuwa wabibi zake na kutumika kikabila na katika ubaguzi mkali. Ni hapo wanafunzi hao walioshirikiana na ndugu Bashizi kaomba basi ndugu huyo Léopold Shimba Lubilanji kuondolewa madarakani bila kupita mda mrefu.

Lakini mambo hayo yote yaonekane kama mengi ni ya uwongo mtupu na nusu kidogo ya ukweli sababu profesa Lubilanji Shimba ni mkorofi anayejulikana na walimu pia wanafunzi wake. Japo hiyo, ni vema tujulishe kama wanafunzi hao wachache waliyotenda mambo kama yale wameficha ukweli sababu kilichowatuma kumtendea ndugu Lubilanji maovu na kuomba kutoshwa kwake madarakani ni mawazo ya kikabila. Wangehitaji ndugu wa kabila lao la Bashi ao yeyote anayesema lugha kama yao ao jirani aongoze masomo ile. Na hata msimamizi wa kamati la kuwatetea wanafunzi wote kapingwa sababu ni wa kabila lingine, kafafanua mwanafunzi Ngobobo Asengula-Wilondja, yule aliyechaguliwa kidemokrasia na wanafunzi wote kufwatana na hatua kachukuliwa na waziri ahusikae na masomo ya juu na univasti inchini mwetu Zaïre. Hatua hiyo yampatia sheria kiongozi wa ISDR na yamtia madarakani bila fujo yoyote ya kikabila, ndugu Ngobobo Wilondja kwa sababu hakuna hatua ingine inayovunja hiyo ya mbele.

Kitu cha kuuzikisha na kusikitikisha zaidi ni kuona kama walimu nao wametajika katika mambo hayo ya haya ya kikabila kunako ISDR/Bukavu. Kufwatana na masemi yake bwana Ngobobo na wafwasi wake wa kundi la wapenda amani, walimu kama vile Bitijula, Buhendwa Wendo, Bagalwa Mapatano na Kazamba pia wanasiasa Jean-Pierre Biringanine na Jean Charles Magabe wamejulikana kuwa wenyi kuwasha moto mkali kunako chuo hicho cha ISDR.

Imata Raphaël Déwen

UHARIRI

Kazi za wakimbizi

Tumesherehekea hapo majuzi kumbukumbu ya Wakimbizi Barani Afrika. Lakini tukichungua kwa kiini hali kwa sasa ya wakimbizi ulimwenguni kutokana na vita viendeshwavyo nchini nyingi toka chuki na ubaguzi wa kikabila kama vile wa rangi na wa kidini, hali yatukia ni ya kitisho na ya uwasiwasi. Imejulishwa kuwa nchini Zaïre, kwa mfano, kwapatikana kwa sasa zaidi ya wakimbizi 900.000 toka nchi 9 jirani.

Ni hasa nchi za Angola, Congo, Uganda, Rwanda, Burundi, Tanzania, Tchad na zinginezo. Na misaada yatolewa haitoshelee. Lakini pia mkimbizi nchini mwao atezamiwa tu kama mkaaji kahamishwa mahali kazaa na hiyo kutokana na vita vilivyoko. Ni wakati tu aenda katika nchi ya kigeni aweza kuhusikiwa na Shirika lihusikalo na wakimbizi duniani. Zaidi ya ubaguzi huo usiokubaliwa na kutokana na haki za msinji zaelekea binadamu, mtu huyo azulumiwa, awe mkimbizi ao anayehamishwa makwake, anayo lazima ya vyakula, ya matibabu, maelimisho na vifaa kazaa.

Nchini Zaïre, ndugu waliofukuzwa jimboni mwa Shaba, Kivu ya Kaskazini na mengineo majimbo wakosewa kabisa makao, vifaa kazaa na vingi na hasa vyakula na maji safi. Wengi kati yao hufariki dunia kutokana na magumu yawatukia ! Kwa sababu kiasi cha vyakula na vinginevyo vyatolewa hakiwezi kuwatoshelea muda wa siku waaminiwa kwani ni kiasi kidogo sana na ambacho hakiwezi kutimizia hata kuku na zinginezo ndege haki zao muda huo waaminikwa. Yasemekana ndugu hao wakimbizi, raãa kama vile wageni wanungunika kwani hawafurahishwe na ginsi misaada yagawanywa ao yatimuliwa kwa manufaa pekee ya wanaokabizwa madaraka ya shuruli. Lakini hujiuliza misaada ya vyakula gani yatolewa ? Ni watu wa utashi mwema ambao katoa misaada hiyo kwa nchi na wengineo wageni ndio wapanga kiasi hicho kidogo hasa cha muhindi, muchele na mengineo ; maharagi, samaki na kazalika. Ingefaa kweli hali ya maisha ya ndugu wakimbizi ichunguliwe kwa karibu na jawabu bora lipatikane ; hasa uchunguzi mkali katika ugawaji wa misaada yatolewa.

Jambo lingine kuhusu haki ya mkimbizi ni maadibisho na maelimisho. Mkimbizi ambaye kajionea namna gani, labda, masomo kafungwa ao kabomolewa na adui ahuzuria, akichomwa moyo, kwa kifo ambacho chafikia mwanae ama ndugu polepole hadi kulazwa. Mwanafunzi wa segondari na wa masomo ya juu hulalamika na kusaga meno kwani apaswa sasa kushika njia ya kuenda shuleni na kuwatizama wakuu na viongozi serkalini asijue nani akaulize apate kumshurulikia. Aomba kulipa masomo na vifaa kazaa !

Wamoja kati ya wote wanaohusika na jambo hilo walalamika kwa sauti kubwa : magumu ni mengi na waomba wawasikie. Lakini sauti yao itasikilika ? Twatumaini na twazani kuwa hao watoa misaada watasikia uchungu na kuwahurumia vijana na wote ambao wachomwa moyo na wakata matumaini. Ndiyo kusema hakuna tena sababu ya kusimulia juu ya haki za mtu na zaidi ya hapo juu ya wakimbizi wa kivita, kama watoto wa wakimbizi hao wapaswa kufa na njaa, kusahau kuenda shuleni ao kukimbizwa huko shuleni kwa kuwa tu amelazimishwa kuacha makwao ambako kapata vyakula na vinginevyo vifaa vyote anavyo lazima.

André Bisimwa L-B Tserou

Jawabu kwa mzozo wa kisiasa nchini Zaïre ni :

Masikilizano na heshima ya mapatano kati ya wanasiasa

Eti Raïs Mobutu akubali kukutana tena na wapinzani lakini...Kwa kweli tukichungua kwa karibu nguvu zaendeshwa kwa kuulaza mzozo wa kisiasa ulioko nchini Zaïre, zote zafikilia tu jawabu moja : masikilizano kati ya wanasiasa na heshima ya mapatano yafanywa na wanasiasa. Wawe wa upinzani kama vile wa upande wa Raïs wa Jamhuri, Mareshali Mobutu. Na hiyo imekamilishwa kweli toka ziara kafanya Askofu Monsengwo Pasinya, prezidenti wa Baraza kuu la Washauri wa Jamhuri, Ulaya, Amerika na Barani Afrika.

Masimulizi rasmi kafanyika kuhusu mzozo huo, imeonekana kuwa kisa chake ni kutokana na kutokubaliana mpaka leo mpango moja ulio bora na wa kudumu. Ni toka hayo, ndipo hapo majuzi Askofu Monsengwo kanena kuwa awapatia bado wanasiasa muda wa kujifikiri na kufikilia masikilizano kati yao hadi tarehe 30 Juni. Na kama mbele ya tarehe hiyo hakuna chochote kimefanyika, basi binafsi atatoa maoni yake kuhusu hali ya kisiasa iliyoko katika hotuba moja muhimu.Popote nchini, watu, katika mikutano, hujuliza na kunongoneza mambo gani Askofu Monsengwo atutayarishia. Ni toka hayo twatoa maoni ya maaskofu wa Zaïre toka mwito wao kafanya kwa wakristu na kwa wote wanao utashi mwema kwa kuokoa nchi yazama katika bahari la magumu.

Katika mwito wao, maaskofu wa Zaïre waomba kwa makanisa wategemee zaidi faida ya raïa pahali pa faida zao wenyewe na madaraka wagombania. Bali pia maaskofu wa dini ya kikatoliki nchini Zaïre waonya kuwa ni muhimu kutoa mwito haraka kwa kuiondoa taifa letu katika hatari. Ni hivi wawatia raïa moyo na wawaalika kumtumainia Mungu. Kuhusu mwito wao kwa wanasiasa, maaskofu hao wataka kuwakumbusha kuwa si lazima tu kusema kwa sauti kubwa kama waunga raïa mkono na wawatumikia ! Yafaa kweli kujiweka katika njia ya sheria na ya uhaki kwa kufikilia maendeleo ya kweli ya raïa wote, waume kama vile wake na nchi yetu ya Zaïre kwa jumla.

Kwa kweli, utafuti na utimizo wa madaraka kwa manufaa ya mtu mwenyewe ni mambo ya kuigeuza siasa kuwa mbaya. Pia, katika muda huu wa mpito, viungo vyote na wanasiasa wote nchini mwetu waheshimu kanuni na viungo kasimikwa na raïa kakutana pamoja kwenyi Mkutano mkuu wa kitaifa. Ni katika viungo hivyo kwapaswa kuwazwa na kuendeshwa madaraka ya kisiasa. Hiyo ni kwa kufikilia raïa ndugu zetu waishi na ujio wao katika udemokrasia. Kulingana na oni hilo hilo, ili kuepuka uchaguzi usiwe na magendo, yafaa katika muda wote wa mpito kusiwe vita, magomvi, mpito uongezwe kuambatana na mahitaji, maoni na hatua kachukuliwa kunako Mkutano mkuu wa kitaifa ili kufikilia kutuliza watu na kuwaadibisha kisiasa na kidemokrasia. Zaidi ya hayo, wanasiasa wangepaswa kujiuliza sababu gani wataka kuchukua madaraka, vyeo na viti na kuweka kuaminisha raïa kuhusu umuhimu wa ratiba lao kisiasa.

Kuhusu hali ya kisiasa iliyoko nchini Zaïre, yasemekana kuwa Raïs Mobutu yupo tayari na akubali kukutana na vikundi vya upinzani ili kutatua matatizo yaliyoko na kutafuta majawabu. Laki Mareshali Mobutu kajulisha kuwa masimulizi yao yafaa yaelekee hasa uchunguzi kwa karibu wa maelezo ya hali ya kika tiba kuhusu mpito, kusimikwa kalendari ya uchaguzi pia kutajwa kwa waziri mkuu wa serkali ya mpito ambaye akubaliwa na vikundi vyote vya kisiasa. Na inafaa nchi za Mangharibi zimsaidie kufikilia pendekezo hilo, wasema.

André Bisimwa L-B. Tserou